



## **BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

### **ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

### **BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI**

### **MKUTANO WA TISA**

**Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 22 Februari, 2018.**

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi  
na Dua itasomwa.

#### **I. TAARIFA YA SPIKA:**

#### **II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

#### **Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC):**

Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC) ya mwaka 2017/2018.

#### **III. MASWALI:**

#### **Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:**

49. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde)  
- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Kwa kuwa Serikali ilifanya zoezi la ukaguzi kwa ajili ya kubaini wafanyakazi wake kwa wizara mbali mbali kwa lengo la kujiridhisha na kuweza kujua mahitaji halisi ya wafanyakazi ambao wanahitajika kwa Wizara

na mashirika yake. Na kwa kuwa wapo wafanyakazi waliostaafu na wanaofariki kwa kila mwaka.

- (a) Je, ni lini kwa mara ya mwisho Serikali ilifanya ukaguzi kwa wafanyakazi wake wa Serikali na mashirika
- (b) Je, ni wafanyakazi wangapi waliostaafu sambamba na waliofariki dunia kwenye Wizara na mashirika hayo kutoka 2015/ 2017
- (c) Je, ni wafanyakazi wa ngapi walioajiriwa ili kujaza nafasi zilizowachwa wazi na watu waliostaafu na waliofariki dunia kwa kipindi cha 2015/2017.

**Wizara ya Ardhi, Maji Nishati na Mazingira:**

- 9. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde)  
- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:

Kaskazini mwa Ofisi ya Kamisheni ya Ardhi Pemba, kuna kiwanja cha mtu binafsi ambacho bado hajakiendeleza. Kutokana na ufinyu wa Ofisi ya Kamisheni, kuna haja ya kujenga Ofisi nyengine itakayokidhi haja.

- (a) Je, Wizara ina mpango wa kufanya makubaliano na mtu huyo ili eneo hilo ipatiwe Kamisheni ya Ardhi Pemba na waweze kujenga Ofisi ambayo itakidhi mahitaji na kutatua tatizo linaloikabili Kamisheni hiyo kwa hivi sasa.
- (b) Je, Wizara ina mpango gani wa kuliboresha jengo la Ofisi hiyo kwa Pemba na kulifanyia marekebisho kwa ujenzi wa vyoo na uzio.

**Wizara ya Afya:**

73. MHESHIMIWA SIMAI MOHAMED SAID (Jimbo la Tunguu) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kwa kuwa kumekuwa na ongezeko la watu wenye ugonjwa wa akili kutembea huru bila ya uangalizi na huduma za hospitali.

- (a) Ni kwanini watu hawa hawapatiwi msaada wa huduma za afya.
- (b) Ni utaratibu gani Serikali inaoutumia kuwalipa fidia au hasara wanayoipata wananchi pale panapotokea uharibufu unaosababishwa na wagonjwa hawa wakati wakitembea huru.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:**

62. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHANI SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Serikali inastahiki pongezi kwa kununua meli za kisasa “digital na electronic”. Hata hivyo, kumekuwa na matatizo ya kiufundi pale meli hizo zinapoharibika ambapo hutafuta mafundi.

- (a) Je, tuna mafundi wangapi wa fani ya “Electronic” katika Shirika la Meli na wangapi waliokwenda kusoma.
- (b) Nini mpango wa Serikali wa kuwasomesha wafanyakazi wa meli wa kozi zote za Meli.

63. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHANI SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Pamoja na jitihada za Serikali katika kupatikana kwa usafiri wa kisasa, bado kuna tatizo kwa safari za Pemba – Tanga, tatizo linalopelekea watu kupanda

vyombo visivyo salama na pia kuikosesha Serikali mapato na kuzidi shughuli za magendo.

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa usafiri wa Tanga - Pemba - Tanga.
- (b) Kwa hali hii inayoendelea ya usafiri wa Pemba – Tanga, Serikali imechukua hatua gani za dharura.
- (c) Je, hatuoni kama pasipokuwa na usafiri wa uhakika ndio tumehakikisha majahazi kubeba abiria na ni hatari.

**IV. HOJA ZA KAMATI:**

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC):**

Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC) ya mwaka 2017/2018.

Zanzibar,  
22 Februari, 2018.

**(Raya Issa Msellem)**  
**KATIBU WA BARAZA.**